




SOLSTICE


Mtifuko wa maji ya bahari, mifumo ya ikolojia ya bahari na jamii ya watu wa pwani



TANZANIA FISHERIES RESEARCH INSTITUTE (TAFIRI)




Mtifuko wa maji ya bahari kuja juu (mzunguko wa maji toka kwenye sakafu ya bahari kuja juu) ni utiririkaji wa maji baridi yaliyojaa virutubisho vingi kutoka kina kirefu kuja juu ya bahari




Mtifuko wa maji ya bahari (mzunguko wa maji toka kwenye sakafu za bahari kuja kwenye tabaka la juu la maji ya bahari) unaweza pia kutokea katika ukanda mdogo kwa mfano eneo lililopo magharibi mwa Kisiwa cha Pemba ambapo mikondo ya maji inaweza kusababisha hali ya namna hii kujitokeza



UNIVERSITY OF DAR ES SALAAM INSTITUTE OF MARINE SCIENCES



Mtifuko huu huleta virutubisho vinavyochangia kukua kwa vimelea maji (phytoplankton) ambavyo ndiyo huwa lishe kwa samaki wanaoishi kwenye safu ya maji ya juu baharini (pelagic fish)



Mtifuko wa maji ya bahari unaweza ukasababisha eneo husika kuwa na samaki wengi, na hivyo kuchangia kuboresha maisha ya jamii ya watu wa pwani katika eneo hilo




National Oceanography Centre

www.solstice-wio.org



Mtifuko wa maji ya bahari (mzunguko wa maji toka kwenye sakafu za bahari kuja juu) unaotokea katika ukanda mkubwa katika maeneo mbalimbali ya mwambao wa Afrika Mashariki hutokea katika misimu yote miwili, yaani msimu wa pepo za kusi na msimu wa pepo za kaskazi



Kiwango na mahali unapotokea mtifuko wa maji ya bahari hubadilika mwaka hadi mwaka kama ambavyo misimu ya pepo za kusi na kaskazi inavyobadilika. Hii inasababishwa na mabadiliko ya tabia nchi

Jamii ya samaki wadogo wadogo elezi kama vile vibua na dagaa ni chanzo kikubwa cha uhakika wa chakula kwa watu wanaoishi maeneo ya mwambao. Pia shughuli za uvuvi hutoa ajira na fursa nyingi za kiuchumi.

Ili kuweza kutunza samaki waliomo tunahitaji kuelewa maeneo yaliyo na hizi tabia za mtifuko wa maji ya bahari na jinsi gani yanavyobadilika mwaka hadi mwaka. Hii itatusaidia kutabiri nini kinachoweza kutokea kutokana na mabadiliko ya tabia nchi na namna ya kujiandaa kuchukua tahadhari kwa ajili ya chochote kinachoweza kutokea siku za baadaye.

Maarifa toka kwa wavuvi wa eneo husika kuhusu mazingira ya bahari ya eneo hilo husika yanaweza kutoa taswira au taarifa muhimu katika usimamizi na uangalizi. Taarifa za namna hii pia zinaweza kutoa mwelekeo wa aina za tafiti za kisayansi zinazotakiwa kufanyika.

Toa taarifa ya mahali utakapoona yafuatayo:

